

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

Simu: +255-22-2133964,
2133969, 0800 110063
Barua Pepe: info@nhif.or.tz
Tovuti: www.nhif.or.tz
Nukushi: +255-22-2133972,
2133982



Makao Makuu,
Tambukareli, Barabara ya Jakaya
Kikwete,
S.L.P. 1437, Dodoma
Tanzania

TAARIFA KWA UMMA

KUFANYIKA MABORESHO YA MIFUMO YA TEHAMA YA NHIF KUANZIA TAREHE 1 HADI 4 APRILI, 2022

Dodoma, Jumamosi Machi 26, 2022:

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unatarajia kufanya maboresho kwenye mifumo yake ya TEHAMA kuanzia tarehe 01 hadi 04 Aprili, 2022. Uboreshaji huu unafanyika ili kuendana na maagizo ya Serikali ya kuhakikisha mifumo inaboreshwa na inasaidia katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Maboresho haya hayatarajiwi kuathiri shughuli za kiutendaji zikiwemo za kuhudumia wanachama wa Mfuko, usajili wa wanachama, uwasilishaji michango na shughuli zingine.

Hata hivyo, endapo kutatokea changamoto yoyote kwa mdau wa Mfuko katika kipindi hicho awasiliane na Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Mfuko kupitia namba **0800110063**.

Aidha Mfuko umejipanga kuhakikisha wadau wake wanapata huduma zote bila ya changamoto yoyote.

Imetolewa na;


Anjela Mziray
MENEJA UHUSIANO